Kufanya Uamuzi

na

Ellis P. Forsman

Kufanya Uamuzi

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Kufanya Uamuzi

Matt. 6:24

Mat. 6:24, "*Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu; ama atashikama na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.*"

Mwanadamu anauchaguzi.

- Katika kuamua mambo ya kimwili ya maisha haya.
- Ama kwenda chuoni, au hapana?
- Kazi ya aina gani mtu anaweza kupambana nayo ili kupata mahitaji?
- Wanaoweza kuchagua wenza wa maisha haya?
- Ama kukodi au kununua?

Haya ni baadhi ya maamzi ambayo tunapaswa kufanya, lakini tunafanya maamzi madogo kila siku.

- Je napaswa kuamka kutoka kitandani sasa, au kulala kwa dakika chache?
- Ni nguo gani nitavaa?
- Nitakula nini asubuhi hii?

Katika kuamua mambo ya kiroho, mwanadamu anapata uamzi, uamzi huo anatakiwa aufanyie zoezi katika kufanya uchaguzi wa mambo ya kiroho.

Watu lazima wachague kati ya mambo mawili muhimu ya kiroho: mmoja anaweza kuchagua kuishi maisha ya kipekee yaliyo thibitishwa, au mwingine anaweza kuchagua kuishi maisha ya kipekee yaliyodharauliwa.

Uchaguzi unaweza kufanywa katika moja ya mapendekezo makuu mawili.

- Mmoja anaweza kuchagua kwa kuzingatia, kuamua, na kulifanyia zoezi uamzi binafsi na kujifunza mapendekezo yaliyowekwa mbele yako.
- Au, mmoja anaweza kuchagua kwa kukataa kuzingatia, kukataa kuamua, na kuruhusu mazingira fulani na msukumo wa kupendekeza uchaguzi wake.

Kukataa kuamua ni mfumo wa uamuzi.

Nikinukuu kutoka kwa William Jennings Bryan: “Kudura sio swala la uchaguzi; sio kitu cha kusubiria, bali ni kitu cha kitimiza.”

Yesu akisisitiza kwamba watu lazima wafanye uchaguzi: Mat. 6:24, “*Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili: kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu, ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kutumikia Mungu na mali.*”

Kwa sababu kuna mgongano wa kupenda kati ya mambo mawili.

Kile ambacho ni sugu ni mambo ya mwili, siyo ya uungu, na dhambi. Inaongelea vitu ambavyo vinasababisha mwanadamu kuweka maana potofu ya ulinzi katika hivyo, au kusababisha mwanadamu kutoa moyo wake kwao badala ya Mungu, au kutengeneza utumwa kwa mwanadamu ambao unaweza kumwondoa katika mwongozo wa Mungu.

Umuhimu wa uamzi huu

Inasisitizwa na Yesu katika kukabiliana kwake na kijana tajiri wa: Marko 10:17-22, “*Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio, akampigia magoti, akamwuliza Mwalimu mwema nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele? Yesu akamwambia kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliyemwema isipokuwa mmoja, ndiye Mungu. Wazijua amri, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu baba yako na mama yako. Akamwambia mwalimu haya yote nimeyeshika tangu utoto wangu. Yesu akamkazia macho akampenda, akamwambia umepungukiwa na neno moja. Enenda ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate. Walakini yeye akakunja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.*”

Kijana mdogo akaja kwa Yesu kwa upole akitamani uzima wa milele.

Anadhihirisha kwamba Yesu ana mamlaka sahihi ya kujibu swali.

Amekuwa makini katika maisha ya dini yake, maana Yesu alipojibu, “Wazijua amri,” akajibu nimeyashika haya yote tangu utoto.

Lakini, kulikuwa na thawabu kuu aliyoambiwa kufanya, akenda akiwa na huzuni, kwa sababu alikuwa hapendi kufanya uchaguzi huo.

Hakuwa tayari kuachia vitu vya muda mfupi alivyopenda.

Watu leo wanakwenda kanisani, na kufikiri kuwa wenye haki, lakini hawafanyi wajibu huo unao watenganisha na dunia.

Uchaguzi kwa Yesu haupaswi kuwa wa kupita; inapaswa kuwa inayotenda kazi, ikihusisha uchaguzi. Mt. 12:30, “*Mtu asiye pamoja nami yu kinyume changu; na mtu asiyekusanya pamoja nami hutapanya.*”

Siyo tu mtu anapaswa kumpinga Yesu ili awe kinyume naye.

Uamzi mgumu

Ilikuwa ni juu ya huyo kijana tajiri (hapojuu). Yesu tayari alikuwa anajua ugumu wa uchaguzi huo. Ilikuwa ni uamzi mgumu kwa Myahudi kuwa Mkristo.

Hii ilikuwa ni kweli kwa uamzi wa kijana tajiri, pia. Kwa sababu hii ingemaanisha kukataliwa na desturi za Kiyahudi.

Dini ya Kiyahudi haikuwa tu dini, bali pia musingi wa taifa, umuhimu wa mila.

Yesu alijua kwamba kwa Myahudi kuukubali Ukristo, atateswa na majirani zake, na atatengwa na familia yake, na kuchukuliwa kwamba amekufa na watu wake mwenyewe.

Katika kanisa la kwanza wengi wa Wakristo hao wa Kiyahudi walipelekwa magerezani na kuawa. Walikuwa na uamzi mgumu.

Msalaba ulikuwa unaogopwa na ishara ya aibu katika siku za Yesu. Kusulubiwa kilikuwa ni kiwango cha kutokuwa na neema; na mtu alibeba msalaba pale tu walipokuwa wanakwenda kusulubisha.

Uamzi wa kumfuata Yesu ulikuwa, na ni uamzi wa kubeba msalaba binafsi, uamzi mgumu wa kukataa aibu na kutokuwa na utu kwa wengine. Kama mtu kwa nia njema hawezi kufanya uchaguzi huo, hawezi kuwa mwanafunzi wa Yesu.

Uamzi kati ya mawazo mawili, nafasi ya kiroho inasisitizwa katika neno la Mungu katika misamiati mingi.

- Uamzi kati ya giza na nuru.
- Uamzi kati ya roho na mwili.
- Uamzi kati ya akili ya roho na akili ya mwili.
- Uamzi kati ya haki na kutokuwa haki.
- Uamzi kati ya mema na mabaya.
- Uamzi kati ya matunda ya roho na matendo ya mwili.

Zingatia umuhimu wa uamzi huu

Rum. 6:1-23, "*Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ubatizo katika*

mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utu weyu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena; kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi. Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye; tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena. Maana kwa kule kufa kwake aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake amwishia Mungu. Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu. Basi dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tama zake; wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silahaa za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki. Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema. Ni nini basi? Tufanye dhambi kwa sababu hatuwi chini ya sheria bali chini ya neema? Hasha! Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki. Nasema kwa jinsi ya kibinadamu kwa sababu ya udhaifu wa miili yenu. Kwa kuwa kama mlivyovitoa viungo vyenu vitumiwe na uchafu na uasi mpate kuasi, vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu vitumiwe na haki vipate kutakaswa. Kwa maana mlipokuwa watumwa wa dhambi, mlikuwa huru mbali na haki. Ni faida gani basi mliyopata siku zile kwa mambo hayo mnayoyataharikia sasa? Kwa maana mwisho wa mambo hayo ni uharibifu. Lakini sasa mkiisha kuwekwa huru, na kuwa mbali na dhambi, na kufanywa watumwa wa Mungu, mnayo faida yenu, ndiyo kutakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele. Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Bwana wetu."

Paulo anawakumbisha utofauti wa kubatizwa kwao kwa kueleza kwamba ubatizo unaonyesha kifo cha dhambi na kiingilio katika Kristo. Kwa kuchagua kumwingia Kristo kwa ubatizo, waliifia dhambi, wakiendelea katika maisha katika dhambi nje ya swali kama wangebaki katika Kristo.

Walifanya uamzi wa kutokuendelea katika dhambi ili kwamba waweze kuishi ndani ya Kristo.

- Mustari wa 11 unaweka wazi kwamba lazima waelewe kwamba wameifia dhambi, na kuwa hai katika Kristo.
- Mustari wa 12-14 inaeleza kwamba hawapaswi kuruhusu dhambi iwatawale, au kuruhusu wao wenyewe kutumiwa kama silaha za dhuluma.
- Neno ambalo lonaweza kuwa hotuba kwa hawa Warumi ni, "Mmefanya uamzi wenu; sasa muishi sawasawa na kwa kuwajibika katika uamzi wenu."

Rum. 8:1-13, "*Sasa basi hakuna hukumu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho. Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waufuatao roho huyafikiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo huyo si wake. Na Kristo akiwa ndani yenu mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi, bali roho yenu I hai, kwa sababu ya haki. Lakini ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu. Basi kama ni hivyo ndugu tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili; kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi.*"

Angalia ulinganifu katika maandiko haya kati ya mtu anayeishi maisha yake katika tama ya mwili, na mtu anayeishi maisha yake kwa mapenzi ya Roho.

- Mustari wa 4-5. wale wanaoishi kwa ajili ya mwili "wanapenda mambo ya mwili," bali wale wanaoishi kwa mambo ya roho hupenda mambo ya Rohoni.
- Mustari wa 6. Mapenzi ya mwili uzaa kifo cha kiroho, bali mapenzi ya Kiroho huleta uzima wa kiroho na amani.

- Mutari wa 7-8. Mapenzi ya mwili hukaa kama adui wa Mungu, haiwezi kumtii Mungu, na haiko tayari kumpendeza Mungu.
- Mmoja anaishi kwa ajili ya mwingine, lakini sio kwa wote.

Kama Wakristo lazima tuwe na toba.

Tunabeba majukumu mathubuti ya kuyachunguza maisha yetu na shughuli zetu kujua kama tunaishi na kuenenda kwa kutii kwa Kristo.

Tabia chache ni hatari zaidi kwa Mkristo kuliko tabia, "sijali kile anachosema Mungu, na sijali Yesu anataka nini; chake ndicho ninachotaka na kukipenda, na nitafanya kama inavyonipendeza.

Tabia hii ni kukana kwa wazi majukumu ya kutii. Ama tunaikumbuka au hapana, tunapoishi kwa tabia hizi, tumeharibu uamzi wetu wa kuishi ndani ya Kristo.

Ufu. 3:14-19, "*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika; haya ndiyo anenayo yeye aliye, Amina, shahidi aliyemwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Nayajua matendo yako ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi, kwa kuwa uana uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu. Kwa kuwa wasema mimi ni tajiri, nimejitarisha wala sina haja ya kitu, nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, kipofu, na uchi. Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako upate kuona. Wote niwapendao mimi nawakemea na kuwa rudi; basi uwe na bidii ukatubu.*"

Kanisa la Laodikia ni mfano mzuri wa umuhimu wa uchaguzi.

Hawa ni watu waliochagua maisha yao katika Kristo, na ambao walikuwa hawaishi maisha ya kuwajibika katika uamzi wao.

Walifiri kwamba yote yalikuwa sawa, na hawakuhitaji chochote. Hii bila shaka ili jumuisha maisha yao ya kiroho pia. Lakini, Yesu anasema walikuwa wanyonge, wenye mashaka, masikini, kipofu, na uchi.

Mistari 15-16. Bwana akasema kuwa walikuwa sio baridi wala moto, bali walikuwa vuguvugu. Akapenda kuwa ni heri wangechagua kitu kimoja. Kama wangeendelea katika hali ya uvuguvugu, Bwana angewatapika watoke katika kinywa chake.

Watu hawa waliandaa kupoa kiroho pamoja na kuwa kiroho. Ukweli ndio ilikuwa kupooza kwao ambayo ingesababisha Bwana kuwatapika. Bwana akasisitiza umuhimu wa kuishi maisha ya kuwajibika katika uamzi uliofanywa kwa ajili yake.

Kuishi kwa ajili ya Kristo siyo kazi muda kidogo.

Kila mmoja wetu kama Wakristo lazima tukumbuke kuwa tunaishi kwa au upande wa Kristo wakati wote.

Hatuwezi kuishi kwake kwa muda mfupi, na upande wake kwa wakati mfupi.

Hatuwezi kuishi kwake katika mambo ya ibada, na kinyume chake katika mambo ya starehe.

Hatuwezi kuishi kwake katika mafundisho, na kinyume chake katika mahusiano na mtazamo.

Kuna njia moja pekee ambayo tunaweza kuwa upande wa Bwana, na hiyo ni kuwa na huai katika kuishi kwake na kufanya mapenzi yake katika mambo yote, katika mazingira yote. Kitu kingine ambacho kimepungua ni pingamizi dhidi ya Kristo.

Vipi kama watu wangeshuhudia tukio la Kristo miongoni mwa Wakristo wengi waliotangazwa leo?

Kimsingi angekatishwa tama kukuta idadi kubwa ya watu waliozuia maisha ya kiroho katika sehemu kadha ya maisha yao.

Waulize watu wamuelezee “Mkristo mwaminifu” na uangalie jibu linalotolewa.

- Kwa wengi, Mkristo mwaminifu sio zaidi ya yule anaye kwenda kanisani kila mara kuabudu.
- Kwa wengine, ni yule anayeabudu na kuepuka dhambi, kama vile ulevi, wizi, kuuwa, uzinzi, na kutumia lugha zisizofaa.
- Wengine wanaweza kuongeza majukumu ya kusoma Biblia kila wakati nay a kuomba wakati wa shida.
- Bado, watu awa hawa, Ukristo hausiki na kazi ya mtu, kidogo inahusika na jinsi anavyofanya kazi, lakini haihusiki na anavyotumia pesa anazopata, na pia haihusiki na marafiki anaowachagua.
- Kwa kweli, katika mawazo ya wengi wajiitao Wakristo, Ukristo hauhusiki kwa asilimia 80% ya maisha yao ya kila siku.

Ukristo hautawali sehemu za maisha ya mtu. Bali unatawala uwepo wake wote katika ukamilifu.

Rum. 12:2, "*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.*"

Kufanyika Mkristo sio swala la kutengeneza mambo machache katika maisha ya mtu na kukubali majukumu machache mapya. Hivyo kumalizika ndiyo kubadilika, maisha ya awali katika dhambi inatazamwa kwamba "yameshapita".

2 Kor. 5:17, "*Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya.*"

Utu wa kale haupo tena, kwa sababu ameuwa tamaa za zamani katika mwili wake, na zimekoma kuishi.

- Efe. 4:22-24, "*Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tama zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.*"

- Gal. 5:24, "*Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake.*"

Mabadiliko yapo mbali kiasi gani?

Kol. 3:17, "Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote kwa jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye."

Uwepo mpya unarekebisha yote tuyasemayo na kufanya. Pia inarekebisha kile tunachoruhusu akili zetu kufikiria.

Pia inarekebisha maamzi tunayofanya kuhusu tunacho kula au kunywa.

1 Kor. 10:31, "Basi mlapo au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu."

Mkristo anapaswa kuwa matakatifu

1 Pet. 1:16, "*…imeandikwa, muwe watakatifu; kama mimi nilivyo mtakatifu.*"

"Takatifu" inamanisha "aliyewekwa pembeni."

"Takatifu" humaanisha "aliyechaguliwa." Inapatikana mara 62 katika Agano Jipya.

"Takasa" inamanisha kufanywa mtakatifu, au wakifu."

"Usafi" na "nadhifu" inatokana na neno ilo hilo la Kiyunani, "hagnos." Inamaanisha "safi, nadhifu" na inaweza kumaanisha kimwili, kidini, au

uasafi wa tabia. Agano Jipya inafunga kwa msisitizo katika umuhimu wa usafi wa Kikristo.

"Takatifu", "takasa" na "Safi" ni misamiati yote inayotumika katika kueleza uasili ambayo Mungu anapenda kwa Mkristo.

Utakaso unahudumia katika nyanja nyingi katika maisha ya Mkristo.

Itakuwa ni mwenendo wa kueleza kile anachokipenda katika kufikiria. Mit. 15:26, "*Mashauri mabaya ni chukizo kwa BWANA, bali maneno yapendezayo ni safi.*"

Itakuwa sehemu ya hekima hiyo ya kiroho tunayopokea tunaposoma neno la Mungu. Yak. 3:17, "*Lakini hekima itokayo juu kwanza ni safi tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki.*"

Ni bora Mkristo aliyekomaa kufundisha mabinti wachanga Wakristo kuwasaidia kukuza uwezo wa Koroho. Tito 2:3-5, "Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingiziaji; wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema; ili wawatie wanawake vijana akili wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao; na kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe; ili neno la Mungu lisitukanwe."

Na kwa vijana inaelezwa umuhimu wa usafi. 2 Tim. 2: 22, "Lakini zikimbie tama za ujanani; ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi."

Mfumo wa usafi unasisitizwa katika ulinzi katika maisha ya Mkristo. Inafanya kazi tu pale tunapohakikisha kwamba imepandikizwa katika mioyo yetu. Majaribu yatainuka ambayo ni ya kawaida kutia changa moto kuwajibika kwetu kwa Kristo.

Hitimisho

Chagueni leo ni nani mtakayemtumikia. Kama mkimchagua Mungu, lazima uwe Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu kufanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa katika kidato cha sita na saba (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wangu akaniambia kuwa haamini kama Mungu yuko. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa,

nikachukua nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kuwa anaona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ilikuwa ni nzuri, lakini alikuwa hana uhakika kama Mungu yuko. Lakini ili awe sehemu salama, labda aende kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba amekwenda kanisani na kuishi maisha mema kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna Mungu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia "haiendi hivyo. Unapaswa kumwamini kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba.** Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo. 11:18, "*…Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kutoka katik chumba nyingine, na kufikiria wewe mwenyewe, "Kuna mwizi humu ndani!" unachukua simu ya mkononi, kwa haraka unawaita polisi, ukiwaambia kuwa kuna mwizi nyumbani kwako, na unawapa anuani yako. Muda mufupi unawasikia wamefika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "Samahani; Samahani!" Je msamaha ni wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba na anataka kubadili maisha yake ili kwamba asije akaiba tena. Hiyo ndiyo toba ya kweli. Ni badiliko la akili linalo sababisha badiliko la tendo. Tunatakiwa kufanya hilo kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kiri.** Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba< na kukiri ni "KATIKA" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha, kuelekea kitu fulani; siyo kwamba tayari mtu ameisha kipata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo pekee ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe, alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kuzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi*

sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye." (Mt. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo jema kulifanya. Unaona jinsi Mungu alivyopendezwa Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema "Imekuwa kwetu sisi kuitimiza haki yote." Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake, siyo kwa sababu ya haki yetu.

Hakika, kama hatuja batizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "kwa ajili ya ondoleo la dhambi". Kwa mwingine anapenda kuacha hatua hii muhimu?

Yesu aliagiza kwamba kufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote, mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Unakaawilia nini? Simama, ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana.*" (Mdo. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Rum. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena;*" (Rum. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimanishi “kunyunyiza”. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuziki mwili kwa kuuwekea udongo kidogo; bali tunauzika mwili.

Kama haujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?